**19 Juni 2018**

**Shirika linaloongoza kwenye sekta ya digitali ya afya, D-tree International, limetunukiwa kiasi cha dola milioni 6 za kimarekani ili kusaidia Wizara ya Afya ya Zanzibar kutekeleza programu maalum ya watoa huduma wa afya ngazi ya jamii itakayotumia mfumo wa digitali**

Zanzibar, Tanzania: 19 Juni 2018: Shirika la D-tree International imetunukiwa kiasi cha dola milioni 6 za kimarekani kutoka kwenye shirika la Foundation Botnar pamoja na Mfuko wa Ubunifu wa Maendeleo ya Watu (HDIF) ili kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar pamoja na wadau wengine katika kutekeleza kitaifa mfumo wa digitali wa afya ya jamii, ili kuboresha utoaji huduma wa afya ya mama na mtoto. Watoa huduma wa afya ngazi ya jamii kisiwani Zanzibar watawezeshwa katika utoaji huduma ya afya kwa familia, mama wajawazito na watoto, kwa kuendeleza mfumo wa digitali unaotumika sasa katika programu ya Uzazi Salama inayotekelezwa na D-tree International ikishirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar.


Mtoa huduma wa afya wa ngazi ya jamii katika programu ya Uzazi Salama, akikutana na mama na mtoto mchanga kisiwani Zanzibar, Tanzania. Picha imepigwa na Mark Leong, Shirika la Afya Duniani

Kama ilivyosisitizwa katika azimio lililopitishwa hivi karibuni na Shirika la Afya Duniani, mfumo wa afya wa kutumia njia ya digitali unafahamika kuwa na uwezo mkubwa sana katika kubadilisha mifumo ya kiafya. Kwa kuanzisha mpango wa kitaifa wa digitali, Wizara ya Afya Zanzibar imejiweka kipau mbele katika kutumia teknolojia ya digitali ili kuboresha utoaji wa huduma za afya.

**Kufikiria upya utoaji huduma za afya ngazi ya jamii kwa kutumia mifumo ya digitali ya afya**

Kisiwani Zanzibar, takwimu za vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga zimeendelea kuwa juu, mara nyingi kutokana na ukosefu wa elimu juu ya huduma muhimu za afya, pamoja

na ukosefu wa uratibu kati ya wagonjwa, watoa huduma wa afya, na vituo vya kutolea huduma za afya. Mapungufu haya yanaweza kusababisha familia kuchelewa kutafuta na kupokea huduma za afya pindi hali inapokuwa mbaya: kipindi cha ujauzito, kipindi cha kujifungua na uhudhuriaji wa kliniki kwa watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, D-tree International imekuwa ikishiriakiana na Wizara ya Afya Zanzibar tangu mwaka 2011 katika jitihada za kuboresha utoaji huduma za afya ya mama na watoto wachanga ngazi ya jamiii kwa kupitia programu ya kibunifu ya Uzazi Salama, programu inayotumia mfumo maalumu wa digitali kutolea huduma za afya katika jamii. Kwenye programu hii ya Uzazi Salama, watoa huduma ngazi ya jamii hutembelea familia na kutoa huduma za afya huku wakiongozwa na mfumo unaowekwa kwenye simu. Watoa huduma wanawasaidia mama wajawazito kutengeneza mpango binafsi wa kujifungua salama, kutambua dalili hatarishi na kuwaunganisha kina mama, pamoja na familia zao, na vituo vya kutolea huduma za afya. Data kutoka kwenye mfumo huu hutumiwa na viongozi na wasimamizi wa programu katika kuhakiki na kufanya mabadiliko stahiki ya kuboresha programu. Kufuatia utekelezaji wa programu hii, takwimu zinaonesha ongezeko la asilimia 50 ya idadi ya kina mama wajawazito wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na ongezeko katika ufuatiliaji wa kina mama waliojifungua mara nne zaidi kulinganisha na hapo awali.

Shirika la D-tree International, Wizara ya Afya pamoja na wadau wengine watatumia fedha hizi kupanua mfumo huu wa digitali ili kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto mchanga na kunufaisha sekta ya afya ya mtoto katika ngazi ya kitaifa. Kupitia ushirikiano huu, watu milioni 1.5 wa kisiwani Zanzibar watakwenda kupata huduma bora za afya ya kina mama na familia.



Kukua kwa Programu ya Uzazi Salama ili kufikia watoto wenye umri chini ya miaka mitano kisiwani Zanzibar, Tanzania. Picha imepigwa na Mark Leong, Shirika la Afya Duniani

**Ushirikiano kati ya taasisi za umma na binafsi kuanzia uanzishaji, utekelezaji na tathmini**

**D-tree International** inayofanya kazi kwenye nchi zaidi ya 12 tangu mwaka 2004, ni shirika linaloongoza kwenye sekta ya digitali ya afya ulimwenguni katika kutumia teknolojia ya kisasa, kujenga mifumo ya digitali ambayo inaimarisha mifumo ya afya, inaboresha programu na kutoa mchango mkubwa kwenye sekta ya afya. D-tree International imeonesha kwamba mifumo ya digitali ya afya inaweza kuboresha maamuzi ya kitabibu, kuongeza motisha na utendaji kazi wa mtoa huduma wa afya, na hatimaye kusababisha matokeo bora ya afya.

**Foundation Botnar** ni shirika la Uswisi lililoanzishwa kwa lengo maalumu la kuboresha afya na ustawi wa watoto pamoja na vijana walioko kwenye miji inayokua duniani. Moja kati ya maeneo muhimu ya shirika hili ni kuwekeza katika akili bandia (Artificial Intelligence, AI) na mifumo ya kidigitali inayotoa suluhisho ili kuharakisha mabadiliko ya huduma ya afya ya kisasa inayobadilika kutoka hospitali kwenda sebuleni.

**HDIF** inalenga kuhamasisha maendeleo ya kijamii kwa kufadhili ubunifu katika sekta za elimu, afya, na maji na usafi wa mazingira kupitia shindano la ubunifu na kwa kutoa msaada wa kiufundi. Kati ya washindanaji 137 walioshiriki, HDIF imetoa ufadhili kwa mashirika saba—likiwemo D-tree International—kama sehemu ya awamu yake ya tatu ya Mfuko wa Ubunifu.

**DONDOO:**

**Wizara ya Afya Zanzibar:**
"Wizara ya Afya inafurahi kuendelea na ushirikiano wetu wa muda mrefu na D-tree International ili kukuza na kuimarisha mfumo wa digitali wa afya ya jamii ambao tayari umeonesha uwezo mkubwa katika kuboresha maisha ya wanawake na watoto kisiwani Zanzibar, kusaidia ukusanyaji wa takwimu na kuimarisha mfumo wa rufaa ili kuepuka ucheleweshaji unaopelekea kusababisha vifo vya mama vinavyotokana na uzazi pamoja na watoto."- Dr. Fadhil Abdalla, Mkurugenzi wa Kitengo cha Kuzuia Magonjwa, Wizara ya Afya ya Zanzibar

**D-tree International:**
"Tangu mwaka 2011, tumeonesha kwamba kwa kuwawezesha wahudumu wa afya ngazi ya jamii kupitia mfumo wa kidigitali kisiwani Zanzibar, tunaweza kuboresha utoaji wa huduma, inayopelekea wahudumu hao kuunganishwa kwenye mfumo mzima wa afya, na kuimarisha mchakato wa kufanya maamuzi pamoja na upangaji mipango. Tunafurahi sana kupata nafasi nyingine ya kufanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Afya pamoja na wadau wengine ili kuupanua mfumo huu hata kufikia nchi nzima." – Erica Layer, Mkurugenzi Mkuu, D-tree International

**Fondation Botnar:**
"Tunaona fursa ya kuondokana na ukosefu wa huduma bora za afya na zenye ufanisi, unaosababishwa na ukosefu wa uratibu mzuri kwa kuwekeza katika mifumo ya kidigitali. Mradi wa Zanzibar unaendana na lengo letu la uwekezaji na tunafurahi kushirikiana na D-tree International ili kupanua programu hii yenye mafanikio." – Stefan Germann, Mkurugenzi Mkuu, Fondation Botnar

**Mfuko wa Ubunifu wa Maendeleo ya Watu (HDIF):**

"HDIF inafurahi kusaidia kazi inayofanywa na D-tree International katika kuboresha maisha ya wanawake na watoto Zanzibar. D-tree International imejithibitisha kuwa kiongozi kwenye sekta ya digitali nchini Tanzania na uwezo wa kushirikiana katika kutengeneza mifumo ya teknolojia pamoja na wadau wa Serikali na jamii. Tunatarajia kujifunza kutoka kwa D-tree International na wadau wake na ubunifu huu kupitishwa na Wizara ya Afya."– David McGinty, Kiongozi wa Timu, HDIF

*Programu ya Uzazi Salama kwa sasa inafadhiliwa kwa msaada kutoka kwa wadau wa Saving Lives at Birth (Okoa Maisha wakati wa kuzaliwa): Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Serikali ya Norway, Shirika la Bill & Melinda Gates, Grand Challenges Canada, na Serikali ya Uingereza. Ripoti hii imetayarishwa na D-tree International na si lazima maoni haya yawe sawa na ya wadau wa Saving Lives at Birth.*

**MAWASILIANO:**

Erica Layer
CEO
D-tree International
elayer@d-tree.org
+255 75 525 8988